


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**  
WAKALA WA VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO



**STASHAHADA YA USIMAMIZI WA NYANDA ZA  
MALISHO NA UDHIBITI WA NDOROBO**

**(DIPLOMA IN RANGE MANAGEMENT AND  
TSETSE CONTROL - DRMRC)**



Kimetayarishwa na:

Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)  
Kampasi ya Morogoro  
S.L.P. 603,  
MOROGORO – TANZANIA  
E-mail: [litamorocamp@gmail.com](mailto:litamorocamp@gmail.com)

## UTANGULIZI

Kozi hii ya nyanda za malisho na udhibiti wa ndorobo ilianzishwa mwaka 1980.

Kozi hii inatolewa katika wakala wa vyuo vya mafunzo ya mifugo (LITA) Kampasi ya Morogoro PEKEE. Na hiki ni chuo pekee Afrika Mashariki na kati kinachotoa wataalamu wa fani hii

Chuo kinapokea wanafunzi watanzania na kutoka nchi mbalimbali za Afrika kama vile Botswana, Zambia, Cameroon, Burkina-faso, Gambia n.k.

Lengo la uanzishwaji wa kozi hii ni kutoa wataalamu waliobobea katika Nyanja ya utunzaji na undelezaji wa nyanda za malisho na udhibiti wa ndorobo.

### Umuhimu wa kozi

Utaalamu unaopatikana kutokana na kozi hii unasaidia katika;

- Kuboresha nyanda za malisho na machunga
- Kupunguza au kukomesha migogoro ya wakulima na wafugaji.
- Kupunguza tatizo la ndorobo kwa mifugo na binadamu

Upatikanaji wa wataalamu wa kutosha katika taaluma hii utasaidia kupunguza/kuondoa tatizo la upatikanaji wa malisho kwa mifugo yetu hapa nchini. Hili limekuwa ni tatizo hasa wakati wa kiangazi ambapo mifugo hufa kaw kukosa malisho. Tatizo hili linahitaji ufumbuzi wa haraka ili kunusuru mifugo yetu na kukomesha migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji.



Vilevile wataalamu katika fani hii watasaidia kupunguza tatizo la uwepo wa ndorobo katika maeneo mbalimbali, ambayo yanashindikana kutumika kwa sababu ya uwepo wa wadudu hao.

### Njia mbalimbali za udhibiti wa ndorobo

Ndorobo hudhibitiwa kirahisi kwa kudhibiti mbungo ambaye anawasambaza kutoka mnyama mmoja hadi mwingine. Baadhi ya njia muhimu za udhibiti wa ndorobo ni;

- Kutumia kemikali za kuuwa wadudu kwa kupulizia kwenye maeneo yao ya kuishi (habitats) au kupulizia wanyama pamoja na kutibu mifugo iliyoathirika.
- Kutumia mitego (traps and targets) ambayo huwavutia mbungo, wakigusa vitambaa vyenye dawa wanakufa
- Kutumia mionzi (sterile male technique), ambapo madume ya mbungo huhasiwa ili yasiweze kuchavusha majike.
- Kubadilisha makazi ya mbungo (Habitat modification) ili yasiwe rafiki kwa mbungo kuishi.

**Picha:** baadhi ya mitego ya mbung'o



### Madhara ya ndorobo kwa wanyama na binadamu

- Husababisha ugonjwa wa Naga (ndorobo), ambapo mnyama anakona sana, uzalishaji kushuka na hatima mnyama anakufa.
- Husababisha ugonjwa wa malale kwa binadamu

### VIGEZO VYA KUJIUNGA NA KOZI

Wanaoweza kujiunga na kozi hii ni wale waliohitimisha ngazi ya astashahada ya tiba na uzalishaji wa mifugo (AHPC, CAHP), astashahada ya kilimo na uzalishaji wa mifugo (CALP) na astashahada ya kilimo na mifugo (AGROVET/VET).

Wahitimu wa kozi hii wanaweza kuajiriwa;

- Serikalini kama maafisa nyanda za malisho (range officers)
- katika vituo vya utafiti
- kwenye ranchi za serikali na za watu binafsi.

Pia wanaweza kijajiri kwa kuanzisha mashamba/ranchi za mifugo.

Mhitimu wa kozi hii vilevile anaweza kuendelea na mafunzo ya uendelezaji wa nyanda za malisho ngazi ya chuo kikuu.